# OFISI YA RAIS – TAMISEMI

## HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOLO

SHULE YA SEKONDARI MAKWEMA
S.L.P 2360,
**KILOLO**
10/12/2020

**Kumb. Na. KDC/MAKSS/ADM/2020/0**

**JINA LA MWANAFUNZI.........................................**

**SHULE YA MSINGI....................................................**

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MAKWEMA KIDATO CHA *KWANZA* MWAKA *2021***

**1. UTANGULIZI**

Ninafurahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha **Kwanza** katika Shule hii. Shule ya Sekondari Makwema ipo Kijiji cha **Lukani** umbali wa kilometa 15 kusini mwa mji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo.
Unatikiwa kuripoti **tarehe 10/01/2021**

**2. SARE ZA SHULE**

**i. Wavulana**

i. Suruali 2 rangi ya jani la mgomba (kitambaa Namba moja kimebandikwa hapo juu) chini upana inchi 18 yenye mkunjo, marinda mawili juu ya mifuko ya mbele na mfuko wa nyuma usiwe na zipu.
ii. Mashati 2 meupe mikono mirefu (tetron) siyo mitumba.
iii. Viatu jozi 2 vyeusi vya kamba visivyo na kisigino kirefu
iv. Soksi jozi 2 au zaidi rangi nyeusi
v. Sweta 2 rangi ya jani la mgomba yenye (**V**) upande wa mbele isiyo na maandishi wala michoro.
vi. Shamba dress/ suruali rangi ya kijani (kitambaa kimebandikwa) na t-shirt bluu bahari, ni lazima itavaliwa siku ya Alhamisi na Ijumaa
vii. Bukta moja na fulana yake, rangi ya bluu au nyekundu na raba kwa ajili ya michezo.

**NB: Unashauriwa kuandika jina la mtoto kwa kila nguo unayompa ili kuepuka kuibiwa**

MAKWEMA SECONDARY SCHOOL

ii. **Wasichana**

i. Sketi 2 rangi ya jani la mgomba (kitambaa namba moja kimebandikwa hapo juu) mchono wa sketi uwe na linda boksi na mfuko upande wa kushoto, mkanda wa kiunoni uwe na upana wa inchi 2 na iwe ndefu chini ya magoti
ii. Shati (blauzi) 2 mikono mirefu (tetroni) na siyo mitumba
iii. Viatu jozi 2 rangi nyeusi vyenye kamba visivyo na kisigino kirefu
iv. Soksi 2 au zaidi rangi nyeupe
v. Sweta 2 rangi ya jani la mgomba yenye (**V**) upande wa mbele lisilo na maandishi wa michoro.
vi. Shamba dress gauni la mshono wa solo rangi ya kijani (kitambaa kimebandikwa hapo juu), ni lazima itavaliwa siku ya Alhamisi na Ijumaa
vii. Hijab (nyeupe) kwa wasichana wa imani ya dini ya kiislamu.
viii. Bukta, singland, t-shirt rangi ya bluu bahari/ nyekundu na raba kwa ajili ya michezo.

**NB: Unashuriwa kuandika jina la mtoto kwa kila nguo unayompa ili kuepusha kuibiwa.**

**3. VIFAA VYA KUJIFUNZIA**

i. Daftari kubwa – counter book 12 au zaidi (Quire 2 na zaidi)
ii. Kalamu, penseli, mkebe na rula
iii. Begi la kubebea daftari
iv. Kamusi moja ya kiingereza – Kiswahili
v. Rimu moja ya karatasi A4 kwa ajili ya mitihani mbalimbali
vi. Faili moja kwa ajili ya kuweka taarifa zake.

**4. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti Shuleni.

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya Shule kulingana na ratiba ya Shule ni lazima
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)
d) Kuwahi katika shughuli za Shule na nyingine utakazopewa
e) Kufahamu mipaka ya Shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika Shule hii.

MAKWEMA SECONDARY SCHOOL

f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya Shule
g) Kuvaa sale za Shule wakati wote unapotakiwa
h) Kuzingatia ratiba ya Shule wakati wote
i) Kutunza mali za Umma.

**5. MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE**

a) Wizi
b) Uasherati na ushoga
c) Ubakaji
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi na kubeli
e) Kupigana au kupiga
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma
g) Kudharau bendera ya Taifa
h) Kuwa mjamzito/ kupata mimba
i) Kuoa au kuolewa
j) Kutoa mimba
k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa Shule au watu
l) Kukataa adhabu kwa makusudi
m) Kuwa na simu ya mkononi.

**NB: OMBI MAALUMU:** Wazazi wawalete wanafunzi masaa ya kazi yaani kuanzia saa **2:00 asubuhi** hadi saa **9:00 jioni**. Hatutapokea mtoto nje ya muda huo wala siku ya Jumamosi, Jumapili na siku za sikukuuu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

______________________________

**NEWAS .M. MTENGA**
**MKUU WA SHULE**
**SIMU: 0753 – 729 – 964**

# HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOLO

## SHULE YA SEKONDARI MAKWEMA

MAKWEMA SECONDARY SCHOOL

## FOMU YA KUPOKELEWA SHULENI

## IJAZWE KABLA YA KURIPOTI SHULE

1. Jina kamili.......................................................................................................................

2.Mahali alipozaliwa...........................................................................................................

3. Tarehe ya kuzaliwa......................................................................................................

4. Jina la Mzazi/Mezi............................................................................................................

5. Kazi yake.......................................................................................................................

6. Namba ya simu ya Mzazi/Mlezi......................................................................................

7. Mahali anapoishi Mzazi/Mlezi;   Kitongoji.......................................Kijiji..............................

8. Dini.......................................................................................................................................

9. Kidato ulichopokelewa.....................................................................................

10. Shule uliyotoka..............................................................................................................

11. Shule ya Msingi uliyomaliza darasa la saba………………………………………

12. Shughuli unazopendelea mbali na masomo kama vile mpira wa miguu, mpira wa mikono, riadha, kuimba n.k Taja……………………………………

13. Wilaya unakotoka……………………………Kata…………………………………

14. Saini ya mwanafunzi…………………………………………………………

**NB:** Kama nikihama nitatoa taarifa.........................................................................

**MATUMIZI YA OFISI**

Namba ya Shule (Admission No.).......................................................................

Namba ya mtihani………………………………………………………………

Lete cheti cha kuzaliwa au affidavit kwa uthibitisho.

MAKWEMA SECONDARY SCHOOL

# HALMASHAURI YA WILAYA KILOLO

### SHULE YA SEKONDARI MAKWEMA

### FOMU YA MAHITAJI MUHIMU YA MWANAFUNZI

Weka alama ya tiki **(V)** kama mwanafunzi ameleta kifaa na alama ya kosa **(X)** kama hajaleta kifaa

**JINA LA MWANAFUNZI**...................................................................**KIDATO**............**KUTWA (  )**

| **VIFAA/KIFAA** | | **AMELETA/HAJALETA (V)/(X)** | **MAONI** |
|---|---|---|---|
| i. | Suruali/ Sketi 2 | | |
| ii. | Mashati/blauzi 2 | | |
| iii. | Viatu jozi 2 | | |
| iv. | Soksi jozi 2 | | |
| v. | Sweta 2 | | |
| vi. | Shamba dress | | |
| vii. | T-shirt | | |
| viii. | Bukta 1 na fulana | | |
| ix. | Raba ya michezo | | |
| x. | Track suit | | |
| xi. | Hijabu (waislamu) | | |
| xii. | Counterbook | | |
| xiii. | Kalamu, penseli, mkebe na rula | | |
| xiv. | Begi | | |
| xv. | Kamusi | | |
| xvi. | Rimu moja | | |
| xvii. | Faili moja | | |
| xviii. | Godoro | | |
| xix. | Shuka 2 (bluu bahari/pinki) | | |
| xx. | Blanketi | | |
| xxi. | Ndoo kubwa moja lita 20 na Ndoo ndogo moja lita 10 | | |
| xxii. | Sahani, bakuli, kikombe na kijiko | | |
| xxiii. | Mfagio (chelwa) na Mopa moja | | |
| xxiv. | Sabuni za kuogea na kufulia | | |
| xxv. | Mswaki na dawa ya meno | | |
| xxvi. | Ndala na taulo | | |
| xxvii. | Doti ya kitenge/kanga | | |

MAKWEMA SECONDARY SCHOOL